JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA

SHULE YA SEKONDARI ITILIMA
S.L.P 184
BARIADI
15/12/2020

KUMB.ISS/F1/2021

MZAZI/ MLEZI WA .....

YAH: <u>MAELEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021 ITILIMA SEKONDARI</u>

1.0. Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Itilima ambayo ni ya kutwa na ni ya mchanganyiko **(Wasichana na Wavulana),** hongera sana.
Shule ni ya mchepuo wa **KILIMO** huku ikifundisha masomo yote kumi ya msingi ambayo ni **URAIA, HISTORIA, JIOGRAFIA, KINGEREZA, KISWAHILI, HISABATI, KEMIA, BAIOLOJIA, FIZIKIA** pamoja na **KILIMO.** Masomo yote yanafundishwa kwa Kingereza isipokuwa somo la Kiswahili.
Muhula wa masomo utaanza tarehe 11 / 01 /2021, hivyo unatakiwa kumleta mwanao bila kuchelewa. Hata hivyo utatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 08/ 01/ 2021 kwa ajili ya usajili wa Mwanafunzi.

2.0. <u>MAHITAJI MUHIMU</u>

- Shati/ blauzi 2 mikono mifupi rangi nyeupe.
- Viatu vyeusi vya ngozi jozi 2 kisigino kifupi.
- Soksi jozi 2, nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.
- Mkanda wa suruali mweusi, kwa wavulana
- Bukta/ Kaptula kwa ajili ya michezo (rangi ya blue).
- T- shirt za blue kwa ajili ya michezo kwa wasichana na wavulana.
- Wasichana watatakiwa kuwa na sketi mbili za rangi ya kijani ambazo zitakua ndefu kuvuka magoti (zifike kwenye vifundo vya miguu). Aina ya mshono utaelekezwa pindi unakabidhiwa fomu hii. Aidha mwanafunzi atatakiwa kulinda heshima yake kwa kuvaa nguo zenye staha.
- Wavulana watatakiwa kuwa na suruali mbili za rangi ya kijani. Suruali inatakiwa kuwa na mifuko mitatu, miwili mbele na mmoja nyuma. Vilevile lazima iwe na marinda mawili kulia na kushoto yenye "Turn up" chini pia iwe pana siyo chupa (Model).
  Hakikisha unashona kulingana na maelezo vingenevyo hutopokelewa. Vifaa hivyo vitakaguliwa wakati wa usajili.
- Daftari kubwa 11 (counter books ni nzuri zaidi)
- Dictionary (English)

- Mathematical set moja
- Mwanafunzi aje na mche mmoja wa mti aina ya mchongoma, mwarobaini au mti wowote unaoweza kutoa mbao/ kivuli.

- Pamoja na barua hii nimekuunganishia fomu ambazo zitajazwa kikamilifu kabla ya kukabidhiwa kwa MSAJILI wa wanafunzi.
- Sheria na kanuni za shule zimeambatanishwa. Zisomwe kwa uangalifu mkubwa.
- Medical Examination form zitajazwa na mganga mkuu wa wilaya.

MUHIMU: HATUA ZITACHUKULIWA KWA MZAZI ATAKAYEMCHELEWESHA MWANAFUNZI KURIPOTISHULENI.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU
MUNGU AKUBARIKI

.....

SHIMBI F.S
MKUU WA SHULE
+255 758189471
+255 716105169
+255 682486129

NAKALA

1. MKURUGENZI WA SEKONDARI
   S.L.P 9121
   DAR ES SALAAM

2. MKAGUZI MKUU WA SHULE
   KANDA YA MAGHARIBI
   S.L.P 1025
   TABORA

3. AFISA ELIMU (M)
   S.L.P 4
   BARIADI, SIMIYU

4. MKURUGENZI MTENDAJI (W)
   S.L.P 308
   BARIADI, SIMIYU

SHULE YA SEKONDARI ITILIMA
S.L.P 184, BARIADI
SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

A. SHERIA ZA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa kuepuka kabisa kutenda makosa yafuatayo:-
Haya yanaweza kusababisha afukuzwe shule kwa mujibu wa sheria za Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi

- Wizi wa aina yoyote.
- Ugomvi, Lugha chafu na Kupigana.
- Udanganyifu katika mitihani ya aina yoyote.
- Kujaribu, Kusababisha au kuongoza na kushiriki kugoma kwa wanafunzi.
- Ubakaji.
- Uasherati pamoja na kupatikana na vifaa vya aina hiyo.
- Ulevi wa aina yoyote.
- Uvutaji sigara, bangi na madawa ya kulevya.
- Kuharibu kwa makusudi mali ya shule.
- Kupata au kusababisha mimba.
- Kutoa mimba.
- Kukataa Adhabu kwa makusudi.
- Kudharau Bendera na Wimbo wa Taifa.
- Kutoonekana shuleni miezi mitatu utafukuzwa shule na bodi ya shule.

B. KANUNI MUHIMU ZA SHULE

1. Mwanafunzi anapaswa kuwa mtii, mwenye adabu na mnyenyekevu nyakati zote na popote. Zaidi ya yote awe na nidhamu ya hali ya juu.
2. Mwanafunzi akiwa nje ya darasa asimame na kusalimia kwa heshima na adabu kwa walimu, mgeni yeyote atakayetembelea shule na wanafunzi wenzie.
3. Ni marufuku kuonesha na kujaribu kuonesha mahusiano ya kimapenzi, Wanafunzi wote ni watoto wa familia moja.
4. Ni lazima kila mwanafunzi kuvaa sare sahihi za shule wakati wote wa nyakati za shule.
5. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuonekana kwenye Vilabu vya Pombe, Baa, Kumbi za starehe, na Majumba ya kulala wageni.
6. Ni marfuku kuvaa pete, heleni, kofia, kufuga nywele ndefu na ndevu, makucha, rangi za vidole, na mdomo pamoja na kutochomekea shati.
7. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuongea lugha zisizo rasmi shuleni. Kiingereza ndio lugha ya pekee ya mawasiliano wakati wote shuleni.
8. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni.
9. Ni lazima kila mwanafunzi paoneshe bidii kubwa katika masomo darasani pamoja na mitihani ya mara kwa mara inayotolewa na walimu.
10. Ni marufuku kuletwa au kuja kuchukuliwa na magari, daladala za baiskeli hapa shuleni au pikipiki hapa shuleni. Wanafunzi wote wanapaswa kuja shuleni na kurudi nyumbani kwa miguu au baiskeli za nyumbani ili kujenga ukakamavu.
11. Ni marufuku kutumia vipodozi, kubadilisha ngozi na kuweka nywele dawa.
12. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
13. Kuvaa sare ya shule wakati wote inapotakiwa.
14. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
15. Kutunza mali za umma.

- Kwa mengineyo yote ambayo huna uhakika nayo uliza kwa walimu au viongozi wateule.

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATIONS AND LOCAL GOVERNMENTS
ITILIMA SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM
(***To be completed by a government Medical Officer***)



Picha ya Mwanafunzi
na
mhuri wa Mwl Mkuu S/ Msingi

Student's full name .....

Age ..... years Sex .....

Stool examination .....

Urinalysis .....

Blood count (Red & White) .....

Syphilist test .....

Spleen .....

Mental condition .....

Sight .....

Chest (TB) .....

Pregnancy .....

ADDITIONAL INFORMATION: (Eg Physical defects/ Impairment or Chronic disease requiring special treatment/ Attention)

.....
.....

I certify that, I have examined the above student and recommend that he/ she is fit / unfit to pursue his / her secondary education.
Signed .....
Designation .....

Official stamp .....
Date .....